Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 82 No. 238 | RAB.I-RAB.II 1444 AH | NOVEMBA 2022 | NUBUWWAT 1401 HS | BEI TSH. 700/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Musa akawaambia kaumu yake: Ombeni msaada kwa Allah na subirini. Hakika ardhi ni ya Allah, Atairithisha Amtakaye katika watumishi Wake; na mwisho (mwema) ni kwa wamchao. (Al-A'raaf 7:129)

Jalsa Salana 51 yafunikwa na Maombi ya Huzur

Na **Mahmood Hamsin Mubiru**
Kiwalani, Dar es salaam

Jalsa Salana ya 51 Tanzania kwa fadhila, huruma na Rehema za Allah ilifunikwa na kivuli cha maombi ya Khalifatul Masih V Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba ambaye katika ujumbe wake kwa Jalsa hiyo ya kihistoria iliyoanza tarehe 1 hadi 2 Oktoba 2022 aliomba Allah Aibariki Jalsa yetu kwa mafanikio makubwa na wale wanaoshiriki wapate baraka kubwa za kiroho, waongezeke katika ujuzi na ufahamu wa dini ya Islam. Maombi hayo yalitimia neno kwa neno na kutuongezea Imani na utulivu mkubwa.

Nusura ya binadamu anasisitiza Huzur ni kwa binadamu kutafuta kwa udi na uvumba Taqwa, ni taqwa peke yake inayoweza kuleta mabadiliko, ni mabadiliko hayo yatakayomfanya binadamu afikie shabaha ya kuumbwa kwake. Katika ujumbe wake, Huzur*atba* anatueleza namna ya kuipata shabaha hii kuu ya kuleta mabadiliko katika hulka zetu. Mara baada ya kueleza tatizo anatupa namna ya kulitatua.



Taqwa! Taqwa! hiyo ndiyo dawa anasisitiza Huzur. Na hakuna njia nyingine ya kufikia taqwa bila ya kufungamana, kupenda, kuenzi na kuheshimu taasisi ya ukhalifa wa Kiahmadiyya. Maisha yetu, mafanikio yetu yamefungamana na Ukhalifa. Bila kamba ya Ukhalifa ni maangamio na fedheha. Elimu na ukaribu wetu ni kupitia MTA. Huzur katika ujumbe huo anatuagiza tusikilize hotuba zake za Ijumaa na zinazohusu matatizo mengine yanayomkabili binadamu.

Matayarisho kabambe. Jalsa Gah ya kuvutia. Usafi wa mazingira. Kila kitu kwenda sawa na ratiba. Witikio mwema wa wageni tuliowaalika akiwemo Waziri wa wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mh George Simbachawene, waumini wa Sabato, wageni toka Uganda na Kenya. Maonyesho ya shughuli za Jamaatm vitabu vya Jamaat; yote hayo yakijumlishwa yanatupa taswira ya maombi yale ya Huzur ya "Mafanikio makubwa". Wanajamaat kutoka kila sehemu ya nchi na wengine kwa kukodi gari huku wamevalia mavazi nadhifu walimiminika katika uwanja wa Jalsa Salana Kitonga na kuwa kivutio kikubwa. Kitonga nzima wafanyabiashara, bodaboda, wauza madafu, hao wote waliomba Jalsa iendelee. Kwa ujumla mafanikio yalikuwa makubwa na wote waliofanikisha Jalsa hii wanastahili maombi ili Allah Awape malipo mema.

Huzur pia aliomba; Jalsa Salana hiyo iwaongezee waliohudhuria ufahamu na ujuzi wa dini ya Islam. Shabaha hii ilitimia barabara. Wataalamu wa Jamaat walitendea haki mada walizopatiwa. Utafiti mkubwa ulifanywa na umahiri wa kuwasilisha mada ulioneshwa na kwa ufupi hiyo ilikuwa ni dhifa ya kisomi iliyotuacha tumeshiba. Wapo ambao wameshauri kuwa mada hizi zipewe sura ya kitabu.

Amir na Mbashiri Mkuu,

Endelea uk. 3

Ahmadiyya kisima kisichokauka

Na Rajabu Abasi Mkieti
Ikwiriri-Rufiji

Mwaka huu tarehe 14 Oktoba tumetimiza miaka 23 tangia mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipoaga dunia (Innalihi wainailahi rajiun) sisi ni Mwenyezi Mungu na kwake tuta rejea. Katika kutafakari namna bora ya kumuenzi mwanaharakati na mpigania uhuru huyu nimekutana na nadharia mbalimbali mojawapo wapo wanaoomini njia bora ni kuyaishi kwa kuyatekeleza yale aliyoyasema na yaliyo andikwa katika nyaraka mbalimbali, wapo wanaoona njia bora ni kuandaa makongamano na kutaja sifa



za mwalimu Nyerere. Wakati nikitafakari nadharia hizo na nyinginezo nikapata hamasa ya kutaka kujua ni lipi chumbuko la fikra na falsafa za mwalimu Nyerere. Tafiti yangu ilinilazimu kurudi mpaka shule ya wavulana ya Tabora. Utafiti wangu unapata nguvu kwani Tabora ndio mahali sahihi katika utawala wa ukoloni palipotumika kupika fikra za vijana na sehemu iliyotumika kulinda tawala za makoloni kwa kupandikiza falsafa za tawala za ukoloni kwa vijana wa kiafrika. Nji walioitumia ilikua ni kwa kuwachukua na kumfundisha hasa watoto wa machifu na vijana

Endelea uk. 5

Maisha ya Mtume Muhammad saw **uk. 4**

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Siri ya Mafanikio

Kila tunapowaalika wageni kwenye Jalsa Salna husimama na wakatoa sifa kubwa sana kwa Jumuiya Ahmadiyya kwa zile kazi tunazozifanya za kujenga misikiti, shule, hospitali, kuchapisha vitabu, maji salama na kueneza kwetu ujumbe wa amani chini ya kauli mbiu yetu ya Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote.

Lakini jambo ambalo huwa hawalisemi na tunalazimika kulitaja, ni nini kinachotupa mafanikio yote haya na nini siri ya mafanikio yetu? Jibu lake linahitaji maelezo. Nabii wa Allah anapokuja anapewa majukumu. Majukumu aliyopewa Masih Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ni kurejesha mafundisho sahihi kama yalivyoletwa duniani na Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Nabii huyo asiyeleta sheria alifanya kazi hiyo kwa mafanikio makubwa kwa kuanzisha Jumuiya 1889 na kuandika vitabu vipatavyo 80. Hata hivyo Nabii wa Allah ni kiumbe na ni lazima aonje kifo kwa sababu kazi yake ni ya kudumu na yeye lazima aondoke, tayari anakuwa amekwisha watengeneza waaminio ambao ni wasafi kiasi hiki ya kwamba mapenzi yao ndio mapenzi ya Mungu. Hawa wanapewa heshima ya kumchagua Khalifa ambaye kwa uhakika na kimsingi anachaguliwa na Allah. Mteule huyu wa Allah anaendeleza kazi za Nabii, anakuja kuondoa wasiwasi ulioingia kutokana na kifo cha Nabii na anawarudisha waaminio amani na utulivu. Mafanikio yote haya unayoyasikia yanatokana na kamba ya Ukhalifa.

Khalifa ndiye mwakilishi wa Allah ardhini. Imani yetu ni kwamba maombi yake yanakubaliwa kuliko maombi ya mtu yeyote yule. Hivyo tusisahau kuwaaambia wanaotumwagia sifa kuwa siri ya mafanikio yetu ni Ukhalifa.

Tizama mafanikko tuliyoyapata katika Jalsa Salana ya 51. Muujiza mtupu. Na muujiza huo ni maombi ya Huzur.

Sisi ambao tumepata bahati tuna wajibu wa kuitumia vizuri. Wangapi tunakumbuka kumuandikia Huzur ili atuombee? Wangapi tunatia maana maelekezo anayoyatoa? Ni bahati iliyoje kwamba tunaweza kumuona na kumsikiliza moja kwa moja kupitia MTA. Ni wajibu wa kila Ahmadiyya kuhakikisha anafuatilia hotuba za Ijumaa za Huzur a.t.b.a. na nyinginezo na kutizama vipindi vingi vya manufaa vinavyoonyeshwa na MTA. Jitihada ifanyike ya kuwakaribisha ndugu, jirani ili waweze kujionea muujiza huu wa kielimu ambao unatolewa na MTA.

Uhai wetu. Maendeleo yetu. Mafanikio yetu. Hivi vyote vinatokana na kufungamana na Ukhalifa.

Zaidi ya Tunayoyaona



Mahmood Hamsin Mubiru

Hivi karibuni wanazuoni wetu mahiri, Profesa Isa Shivji, Profesa Saida wameitendea haki taaluma kwa kutupa hidaya adhimu na urithi wa kujivunia kuhusu Maisha na harakati za mwanamajumui maarufu katika Afrika Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Urithi huo umo katika juzu tatu zilizosheheni umahiri wa uchambuzi, ukusanayaji kwa kutumia jicho makini na kufutilia kwa mbali utamaduni wa kusifu hata mahali ambapo hakuna sababu yooyte ya kusifu. Hatuwezi kusema kwamba kazi hii haina upungufu, La hasha! Upungufu ndio mwenendo wetu sisi binadamu, tunachosema jitihada kubwa imefanywa na uadilifu unataka usimdhulumu yule anayestahili haki yake.

Upungufu unaojitokeza unatokana na ile kasumba na maradhi ya kufikiri kila kizuri bila shaka kimetoka nje. Tutajitahidi kueleza upotofu wa dhana hii. Katika juzu hizi tatu hoja ya msingi ni kwamba kila jambo alilolifanya Julius Kambarage Nyerere lilisukumwa na falsafa ya usawa wa binadamu. Huwezi kugusa jambo lolote alilolifanya Mwalimu bila kugusa itikadi hiyo ya usawa wa binadamu. Hili wanazuoni wetu wamefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuweka jambo hilo bayana. Kama Mwalimu alipigania uhuru ni imani kuwa hakuna binadamu aliye bora kumtawala mwingine. Kama aliingia katika harakati za kusaidia wanaodhulumiwa mahali popote duniani ni kwa sababu ya kuamini kuwa hakuna binadamu mwenye haki ya kumnyonya na kumkandamiza binadamu mwingine. Elimu ya kujitegemea, Ujamaa vyote hivi viliendeleza kumuenzi ni kumtukuza binadamu. Jambo la kusikitisha na ambalo hatukubaliani nalo ni hili la kufikiri kuwa falsafa hiyo ya Mwalimu kuhusu usawa wa binadamu ameitoa Chuo Kikuu cha Makerere na Chuo Kikuu cha Edinburg inakodaiwa alikutana na wanafalsafa Rousseau, Voltaire, John Stuart Mill. Adam Smith.

Julius Kambarage Nyerere kabla hajaenda Makerere alikuwa shule ya wavulana Tabora. Ukichunguza sana maisha ya Julius Kambarage Nyerere utagundua uhusiano mkubwa uliopo



Maulana Sheikh Mubarak Ahmad Ahmadi H.A.

baina ya Nyerere na mji wa Tabora. Ni katika mji wa Tabora alipopata elimu yake, katika Tabora akafundisha, ni katika Tabora ulikofanyika uamuzi wa busara wa TANU ikashiriki katika uchaguzi wa kura tatu.

Kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu shule ya Tabora na Julius Nyerere. Walimu wake, vitabu alivyosoma, wanafunzi wenzie aliokuwa nao. Jambo moja tuna uhakika nalo ni kwamba aliathiriwa sana na Mwalimu wake Sheikh Mubarak Ahmad. Wanafunzi hawa wawili Julius Kambarage Nyerere, Kaluta Amri Abedi walimtembelea Sheikh Mubarak Ahmad aliyewaeleza mafundisho ya Islam kuhusu usawa wa binadamu. Sawa na Islam Allah ni Muumbaji wa wote, weusi, weupe, wekundu, kumbe sote tumeumbwa na muumbaji wetu ni yule yule. Aliwaeleza juu ya usawa unaopatikana msikitini. Hakuna nafasi maalum kwa yeyote, anayefika kwanza ndiye anasimama mbele hata kama ana nguo za viraka, heshima ya mtu haitokani na rangi yake bali uchamungu. Siku ya kuanguka kwa Makka usalama na amani vilipatikana kwa kuwa chini ya bendera iliyokuwa inapeperushwa na Bilal r.a. aliyewahi kuwa mtumwa. Ibada ya Hijja inawakusanya watu kutoka kila pembe ya dunia huku wamevaa nguo za aina moja. Wafalme na watu wa kawaida wote wakiwa sawa wakitafuta fadhila za Allah. Walichukua muda wa kuchambua hotuba ya mwisho ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alipoeleza kinagaubaga usawa wa binadamu. Hoja yetu ni kwamba falsafa hii iliyochanua na kumuongoza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ni mbegu iliyopandwa na Mubashir wa kwanza wa Jumuiya ya Ahmadiyya kutumwa Afrika Mashariki, Maulana Sheikh Mubarak Ahmad.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Jalsa Salana 51 yafunikwa na Maombi ya Huzur

Kutoka uk. 1

Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry katika hotuba yake ya Ijumaa hakufanya lolote ila kwa usahihi kabisa alisoma ujumbe wa Kiongozi wetu mpendwa. Yapi yanaweza kuwa maneno bora kuliko yale ya mwakilishi wa Allah ardhini? Katika hotuba ya ufunguzi wa Jalsa Amir na Mbashiri Mkuu alikumbusha tena ujumbe wa Khalifatul Masih. Baada ya ukumbusho huo alitoa shukurani kwa Allah



Sheikh Abdulrahman Ame



Sheikh Khawaja Muzaffar



Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry



Sheikh Karimuddin Shams



Mwl Abdullah H. Mbanga



Ndugu Ramadhan Nauja



Sheikh Shaban Shunda



Sheikh Musa Isa Mashiri

kuwezesha Jamaat Ahmadiyya Tanzania kuwa na Jalsa Salana yake ya 51 kwani kwa miaka miwili 2020 na 2021 haikuweza kufanyika kutokana na maradhi ya UVIKO-19. Amir pia alitoa tahadhari kuwa ingawaje maambukizo yamepungua ya maradhi hayo hatua zinatakiwa kuchukuliwa za kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kujiepusha na misongamano isiyo ya lazima. Jalsa Salana alisema ina shabaha ya malezi ya kihulka. Ndio maana katika Jalsa Salana zinatolewa hotuba za kukumbushana mwamino wajibu wake kwa Allah na viumbe wake. Alitoa mwito kwa waliopewa majukumu wayatimize vizuri kwani walikuwa wanawahudumia wageni wa Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as]. Kwa siku hizo mbili aliwaomba waendelee na maombi, wakumbuke kushikamana na Ukhalifa na njia bora kwa hivi sasa ni kutizama MTA.

Mada za kina zilizofanyiwa utafiti na wanazuoni wa Jamaat zilisadifu vilivyo maombi ya kuwa waliohudhuria waondoke na ufahamu pamoja na ujuzi wa dini. Uchaguzi wa mada nao ulikidhi haja ya matatizo yanayotukabili. Sheikh Asif Bhatt na ubingwa wake ule wa Kiswahili alifurahisha na kutuelimisha juu ya suala lile linalohusu nusu ya dini – ndoa. Nyumba zinayumba. Furaha imepotea kwa kutozingatia mafunzo ya Islam ambayo katika zama hizi yanakumbushwa na Khalifatul Masih. Sheikh Musa



Sheikh Abid Bhatt



Sheikh Asif Bhatt

ibn Isa alisimama na kutueleza kinagaubaga juu ya kukuza mapenzi kwa Ukhalifa kwani bila Ukhalifa nyuma au mbele hakuna chochote isipokuwa giza. Sheikh Shabani Shunda alisema hakuna maendeleo kwa mtu binafsi au nchi bila ya kujitoa waqfu, kuwa tayari kumtumikia Allah wamepata mafanikoi waliojitoa waqfu na tuliobaki tunafaidika kutokana na baraka hizo za kujitoa waqfu. Sheikh Abdulrahman Ame aligusa juu ya fitina kubwa inayosumbua binadamu – fedha. Watu wana mapenzi ya ajabu na fedha na wako tayari kufanya lolote ili kuzikusanya fedha. Lakini fedha za baraka ni zile unazozikusanya kihalali na ukawa tayari kuzitoa kwa ajili ya Allah. Hawapotezi wala hawapungukiwi wale wanaotoa kwa njia ya Allah. Kutoa sio kazi rahisi hadi umelewa na mapenzi ya Allah. Ukishampata Allah ukampenda, ukajenga uhusiano naye kila kilicho kizito kinakuwa chepesi, lakini kumpata Allah kuna mbinu na mikakati na hayo yote yalielezwa kwa ufundi mkubwa na Sheikh Khawaja Muzaffar. Mbora wa kutuonesha mikakati hiyo, njia hiyo ni nani kama siyo Mbora wa viumbe wote, Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. yeye ndiye mfano bora kwetu sote aliyepitia katika kila nyanja ya maisha na huko kote akatuonesha nini cha kufanya. Sheikh Karimuddin Shams kwa mifano hai na ya kusisimua alitubeba kifikra hadi tukamuona Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. akituonesha mfano wake thabiti wa imani yake kwa Allah wakati wa shida na misukosuko.

Katika zama hizi ukipata shida na misukosuko kimbilio ni kwa Ukhalifa. Taasisi ya Ukhalifa ndio tegemeo pekee la Islam. Kwa umahiri mkubwa Ramadhani Nauja aliwakumbusha wale wenye kuhangaika waelewe kuwa Ukhalifa sio ujanja wa watu kukaa na kujichagua. Ukhalifa unatoka kwa Allah na ni yeye ndiye mlinzi wa taasisi hiyo. Ni taasisi yenye baraka tele na mafanikio ni kuungana na taasisi hiyo. Taasisi hiyo ina kiongozi na ina mfumo ambao ni lazima uheshimiwe na ufuatwe. Mfumo huo ndio unaongoza umma na una wajibu. Wajibu huo aliueleza kwa ufasaha Sheikh Abid Mahmood Bhatt aliponguruma juu ya nafasi na dhima ya viongozi wa Majlis Amila ya Taifa na matawi katika malezi ya wanajamaat. Viongozi wana dhima kubwa nayo si kusema tu bali kusema, kutenda na kuonyesha njia. Bila kuwa mfano mwema huwezi kuleta athari yoyote kwa wale unaowaongoza. Yote hayo yanaweza kupatikana kwa kuogelea katika bahari ya elimu iliyoletwa na Masih Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as]. Na elimu za kimbungu haziji hivi hivi kuna adabu ya kuitafuta. Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alisema Masihi akija atagawa mali, wale wanaofikiri mali hizi hizi wamekosea, mali ni elimu na Masihi Aliyeahidiwa ameandika vitabu takriban 80. Jukumu la kutusaidia tuogelee katika bahari alipewa mtoto wa Pwani Kungwi Abdullah Khamis Mbanga. Palichangamka. Watu wakatabasamu na kufurahi. Na hivi leo hatuna sababu ya kutoogelea kwani vitabu vya kutosha vya Masihi Aliyeahidiwa[as] vimo katika lugha ya Kiswahili. Tutakuwa tumeipata Jalsa Salana ya kweli tukianza kusoma vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as].

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*



Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad[ra] Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

UJIO WA MSAFARA WA KIBIASHARA WA MAKUREISHI NA VITA VYA BADRI

Mnamo mwezi wa kumi na tatu baada ya Hijra, kukawa kunakuja msafara wa kibiashara kutokea Syria, ukiwa chini ya uongozi wa Abu Sufian, ambao kwa kisingizio cha kuuhifadhi, watu wa Makka wakawa wameamua kuleta Madina jeshi kubwa. Mtume s.a.w. pia akawa amepata taarifa ya habari hii na Wahyi wa Mwenyezi Mungu ukamteremkia kwamba sasa wakati umefika dhulma ya maadui ijibiwe kwa silaha zake zenyewe.

Hivyo akatoka Madina akiandamana na wenzake wachache. Alipokwisha toka Madina, hadi wakati huo haikuwa imedhihirika kwamba mapambano yatakuwa dhidi ya msafara ule au dhidi ya jeshi lenyewe. Ndio sababu alitoka Madina akiwa na watu mia tatu. Isifahamike hivi kwamba msafara mradi wake ulikuwa ni ngamia waliokuwa wamesheheni mali. Bali watu wa Makka walikuwa wakituma jeshi imara lililokuwa likiandamana na misafara hiyo. Kwa sababu walikuwa pia wakitaka kuwatisha Waislamu kwa njia ya misafara hiyo. Hivyo kabla ya msafara huu, kuna misafara miwili inayotajwa ndani ya historia kwamba mmojawapo ulikuwa na askari mia mbili wa kuulinda na mwingine ulikuwa na askari mia tatu wa kuulinda.

Hivyo katika hali hizi, ni upotoshaji tu kwa waandishi wa Kikristo kuandika hivi kwamba (Mtume s.a.w.) alitoka Madina akiwa na watu mia tatu kwa ajili ya kwenda kuushambulia msafara usiokuwa na ulinzi wa watu wa Makka. Kwa kuwa msafara huu ulikuwa ni mkubwa sana, hivyo ikilinganishwa na idadi ya askari wa misafara iliyopita, inapaswa kufahamika hivi kwamba ni lazima ulikuwa na wanajeshi mia nne au mia tano hivi.

Kama jeshi la Kiislamu, lililo jumuisha watu mia tatu tu na lililokuwa pia halina hata zana za kivita, lilitoka kwa ajili ya kwenda kukabiliana na jeshi kubwa la kiasi hicho, basi kusema kwamba lilienda kupora, yaweza tu kusemwa kwamba kusema hivyo kunatokana tu na chuki isiyo na sababu, uonevu na utovu wa uadilifu. Kama ingekuwa ni suala tu la kukabiliana na msafara huo, hata hivyo kukabiliana huko kungeitwa kuwa ni vita (sio uporaji) na vita yenyewe ni ya kujihami, kwa sababu jeshi la Madina lilikuwa ni dhaifu na lilitoka tu kwa ajili ya kwenda kuiondoa fitina ile iliyokuwa imewekwa msingi na watu wa Makka ya kuwachochea makabila ya wale walioizunguka (Madina). Lakini kama vile inavyofahamika kutokana na Kurani Tukufu, matashi ya kimbingu yalikuwa pia kwamba mapambano yawe dhidi ya jeshi la Makka badala ya msafara ule.

Na ni kwa ajili tu ya kudhihirisha uaminifu wa Waislamu na imani yao, jambo hili likawa halikudhihirishwa mwanzoni. Wakati Waislamu walipokuwa wameshatoka Madina bila ya maandalizi kamili, basi baada ya kufika kitambo fulani, ndipo Mtume s.a.w. akawadhihirishia Masahaba kwamba matashi ya kimbingu ni haya kwamba, vita ipiganwe na jeshi lililotokea Makka.

Habari zilizokwisha kuja kutoka Makka kuhusiana na jeshi hilo, ilikuwa imefahamika kwamba idadi ya jeshi ilikuwa ni ya askari zaidi ya elfu moja na pia wote walikuwa ni askari wenye uzoefu. watu waliokuwa wamekuja na Mtume s.a.w. walikuwa ni mia tatu tu na kumi na tatu na miongoni mwao pia, walikuwemo wengi waliokuwa hawana fani za kivita. Kisha hawakuwa na silaha za kivita za kutosha. Wengi wao walikuwa wamekuja kwa miguu au kwa ngamia. Farasi alikuwa mmoja tu.

Jeshi hili dogo lililokuwa pia halina nyenzo, kukabiliana na jeshi la maadui lenye uzoefu na lililokuwa na idadi ya mara tatu zaidi yake, lilikuwa ni jambo lenye hatari mno. Ndio sababu hakupenda kumlazimisha mtu yeyote kupigana vita bila ya mwenyewe kuridhia. Hivyo akawauliza wenzake swali hili kwamba sasa hakuna tena swala la kukabiliana na msafara, bali uwezekano ni wa kukabiliana tu na jeshi na kwamba wamshauri kuhusiana na hali hii.

Mmoja baada ya mwingine miongoni mwa Wahaajir (Waislamu waliohamia Madina kutoka Makka) wakawa wanasimama na kusema: Ewe Mtume wa Allah, hata kama adui awe ameparamia juu ya nyumba zetu, sisi hatumuogopi, tupo tayari kupambana naye. Kila alipokuwa akisikia jawabu la kila mmoja aliendelea tu kusema; nishaurini. Hadi wakati huo watu wa Madina walikuwa kimya, kwa kuwa jeshi walilokuwa wapambane nalo lilikuwa ni la ndugu na jamaa wa Wahaajir. Walikuwa wakihofia kwamba isije mioyo ya Wahaajir ikachukizwa na kauli yao.

Wakati Mtume s.a.w. alipoendelea kusisitiza kwamba nishaurini, basi kiongozi fulani wa Waanswar alisimama na kusema: Ewe Mtume wa Allah! Unapata ushauri, lakini yawezekana kusisitiza kwako kuomba ushauri ni kwa ajili yetu wenyeji wa Madina. Mtume s.a.w. akajibu ndio. Kiongozi yule akajibu: Ewe Mtume wa Allah! Labda pengine unatutaka ushauri kwa sababu hii kwamba kabla ya kuja kwako Madina tulikuwa na makubaliano kati yako na sisi nayo yalikuwa hivi kwamba kama yeyote yule akushambulie wewe na Wahaajir ndani ya Madina, basi sisi tutakulinda. Lakini sasa kwa wakati huu umekuja nje ya Madina na pengine mkataba ule unakuwa haugoti kwenye hali kama hii. Ewe Mtume wa Allah! wakati mkataba ule ulipofanyika, hadi wakati huo tulikuwa hatujaupata uhakika wako kwa undani. Lakini sasa wakati ambapo daraja lako na shani yako imeshatudhihirikia kikamilifu, sasa ewe Mtume wa Allah! makubaliano yale si chochote. Sisi hatutakuambia kama walivyosema watu wa Musa kwamba: Idh hab anta wa Rabbuka faqaatilaa innaa haahunaa Qaaiduun Nenda wewe na Mola Wako mkapigane na adui, sisi twaketi hapa hapa. Bali sisi tutapigana kulia kwako na tutapigana pia kushoto kwako, tutapigana mbele yako na tutapigana pia nyuma yako na ewe Mtume wa Allah, yule adui aliyekuja kukudhuru hatoweza kukufikia bila ya kupita juu ya maiti zetu. Ewe Mtume wa Allah! vita ni jambo tu la kawaida. Kitambo kidogo tu kutokea hapa kuna bahari. Tuamrishe kwamba tuwaingize farasi wetu ndani ya bahari nasi bila ya kusita tutawatumbukiza farasi wetu baharini."

Huo ulikuwa ndio ule mfano wa uaminifu na wa kujitolea ambao mfano wake hakuna nabii yeyote aliyepita awezaye kuuonyesha. Mfano wa watu wa Musa watu hao wenyewe walishautoa. Mfano waliouonyesha wanafunzi wa Yesu katika kukabiliana na adui Injili yatoa ushahidi. Mmoja alimuuza mwalimu wake kwa fedha chache tu mwingine alimlaani na kumi waliosalia wakamtelekeza na kukimbia huko na huko. Lakini waliokuwa na mtume wa Allah, Muhammad s.a.w., kwa kuishi naye kwa mwaka mmoja tu na nusu, wakawa wameimarika kiimani kiasi hiki kwamba walikuwa tayari kujitumbukiza baharini kama tu angeagiza hivyo.

Kusudio la ushauri huu lilikuwa ni kwa ajili hii tu kwamba ili wale watu waliokuwa na imani dhaifu waweze kupewa ruhusa ya kurejea (makwao). Lakini Wahaajir na Wa Answar waliopoonyesha mfano wa kushindana katika imani na uaminifu, na makundi yote mawili yakakubaliana kwamba hawataikimbia vita kutokana na kuwepo kwa ahadi ya Mwenyezi Mungu, ingawa idadi yao ilikuwa ni thuluthi ya ile ya maadui na juu ya kuwa na nyenzo chache sana ukilinganisha na walizokuwa nazo maadui, bali wakionyesha ghera ya dini ya Mwenyezi Mungu, watautoa kwa furaha uhai wao katika uwanja wa vita. Hivyo wakaendelea.

Itaendelea toleo lijalo

Ahmadiyya Kisima Kisichokauka

Kutoka uk. 1

waliokua na vipaji katika zama hizo za giza la ukoloni. Na baadae kuwatumia katika kuendesha tawala hizo za kikoloni.Kazi ya kupika vijana haikufanywa tu bora lienda bali ilifanywa na waalimu mahiri na wenye stadi huku ikisimamiwa na mwalimu bwana John Blummer aliyekuwa mwalimu mkuu wa shule ya sekondari ya wavulana Tabora. Mwalimu Blummer ni mwalimu aliyehitimu katika chuo kikuu cha Cambridge ambacho sina haja ya kukielezea kwa watafutao elimu katika zama za leo juu ya ubora na sifa zake. Mwalimu Blummer alitosha kufanya kazi ya usimamizi kwani Shekh Amri anasadifu hili katika kipande cha shairi katika kitabu cha Diwani ya Amri akimsifu mwalimu wao

Blummer once head of our clan,
Many more come to mind,
Many more than I Could name.

Mwalimu Blummer wakati akiendela na kazi yake mara anampokea mwanachuo sio tu mwanachuo bali mwanafalsafa na msomi alihitimi shahada ya lugha ya Kiarabu na anayejua lugha ya Kiingereza kwa ufasaha kinagaubaga. Huyu sio bali ni Shekh Mubaraka Ahmad. Maulana Hakuna na mengi yeye alikuja hapa Afrika ya Mashariki kwa kazi moja tu kuja kuleta ukombozi wa kifikra na hapa shule ya sekondari ya wavulana ya Tabora aliona ndio sehemu sahihi pakuanzia harakati zake. Shekh Mubaraka aliomba kufundisha somo LA dini kwa umahiri wake mwalimu John Blummer hakufanya ajizi akamkubalia na kumpangia kipindi Mara moja.Shekh Mubaraka aingia darasani. Kazi hii ya kuleta ukombozi wa fikra sio rahisi kwani darasa aliloingia lina watu tena wanojua kilicho waleta ni nini kutoka kwao Kuja shule. Shekh Mubaraka alianza somo la dini kwa kuvunja Miungu bandia na kuonesha utukufu wa Mungu wa kweli kuwa ni Mmoja Asiye na mshirika, umahiri wake wakujieleza na utamu wa lugha yake fasaha ulitosha mwanafunzi kuto kukosa kipindi. Moja Kati ya mwanafunzi ambaye hakupitwa na kipindi ni Mwalimu Julius Nyerere.Katika somo lake la dini Shekh Mubaraka alijitosheleza hakuitaji msaada mpangilio wa mada zake uliweza kumaliza kiu ya mwanafunzi juu ya ukweli wa dini. Moja ya hoja alizoweka mbele ya wanafunzi ni kifo cha Nabii Isa as, uhuru wa kuabudi, Haki za binadamu na usawa, haja ya kujitawala, utume kuendelea baadae ya Mtume Mtukufu saw, ukweli wa Hadharat Mirza Ghulam Ahmad as. Sina shaka hata chembe kama Sheikh Mubarak alikua akiaminiwa na wanafunzi wake kwani fikra zake juu ya usawa na utu zinaonekana katika mashairi hata ya Mwalimu Nyerere hasa shairi lake la Usawa wa Binadamu, Mwalimu Julius Nyerere alijipambanua mapema kuwa mpigania uhuru, muumuni wa umajumui wa Afrika, mchukia rushwa, mpenda maendeleo, mlinzi wa rasilimali za Taifa, inatosha kusema mwalimu Julius Nyerere alikua ni Baba wa Taifa baba anahaki zote juu ya kulitunza bali kulilea Taifa kama anavyo andikwa na waandishi mbalimbali wa historia.Wakati wa kupigania uhuru Tanzania mwalimu aliweza kuachaka kazi ya uwalimu tena akifahamu fika atahatarisha imani yake ya dini ya kwa kujiunga na wapigania uhuru watu wenye imani tofauti na dini yake kama anavyoeleza katika vitabu vyake mwalimu wangu wa historia Muhammedi Saidi lakini huwezi kubeza Katu mchongo wa Shekh Mubaraka katika maisha hayo ya siasa kama humfahamu Shekh Mubaraka ambaye amesoma vitabu vya Hadharat Mirza Ghulam Ahmad as kama *Ujumbe wa Suluhu* na *Nyota ya Kaisari* vinavyoweza jenga fikra ya kuvuliana katika kidina na kushirikina katika harakati za maendeleo. Hakika nionavyo mimi maisha ya Mwalimu Julius Nyerere ya natosha kufahamu



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmadas
Masihi na Mahdi aliyeahidiwa

Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya hasa kwa mtafiki yoyote ambaye atasimamia wastwa katika jicho la kuipenda nchi.Kama yupo mtu anayependa kuwa kiongozi bora mchukia rushwa mpenda maendeleo ni wajibu wake kuvisoma vitabu vya jumuiya ya waislamu Ahmadiyya angalau kwa akali basi vitabu vyote vya Hadharat Mirza Ghulam Ahmad as. Mwalimu Nyerere hakuisaha jumuiya ya waislamu Ahmadiyya hata pale alipo Kalia kiti cha Uongozi wa ikulu daima kama alipata jambo la kumtatiza haraka alitafuta Ushauri kutoka kwa viongozi wa jumuiya ya waislamu Ahmadiyya, je Nani hajui hutuba ya Mwalimu Nyerere aliyomtoa jasho Rais Kwame Nkuruma wa Ghana jijini Cairo kama iliandikwa na Shekh Amri Abedi mwanajumiya wa Ahmadiyya na waziri katika serikali ya mwalimu



Rais Kwame Nkrumah

Nyerere.Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ***kisima kisicho kauka*** busara na hekima zake zinatosha kuwa msaada kwa Taifa hili. Kazi hii sio tu ilifanywa kipindi cha uhai wa Mwalimu Julius Nyerere bali hadi Leo kazi hii inaendelea, Tanzania alipofikisha nusu karne katika kujikomboa kutoka mikononi mwa waingereza. Kiongozi wa jumuiya ya waislamu Ahmadiyya Hadharat Mirza Masror Ahmad atba Khalifa tul Masihi V alichonga kalimu kufanya kazi ileile iliyo mleta Shekh Mubaraka katika kuleta ukombozi wa fikra Khalifa tul Masihi V alisema:

"Ni maombi yangu kwamba watu hususan wa Tanzania na Afrika kwa ujumla waweze kutumia vilivyo faida ya uhuru walioupata. Wajitahidi kabisa kutumia raslimali walizopewa kwa ajili ya manufaa ya watu wao. Nchi zote ziweke maanani hadithi ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. isemayo: Kiongozi wa nchi ni mtumishi wa Taifa. Hili ni jambo muhimu la kukumbukwa, sheria zote zinazotengenezwa katika nchi ziwe sawa kwa watu maskini na matajiri, jambo hili likifuatwa basi, Inshallah - Mwenyezi Mungu Akipenda - uhuru ambao mmeupata baada ya muda mrefu sana wa ukoloni na utumwa sasa utadumu. Lakini endapo hamtalifuata hili mataifa makubwa kwa mara nyingine tena yataingia katika nchi zenu na kuchukuwa malighafi zenu kupitia mipango ya udanganyifu na hila ama kwa sababu zozote ziwazo zisizo na ukweli ndani yake.

Kama viongozi wa nchi zinazoendelea wanatimiza haki za watu wao na watu wenyewe wanatoa kipaumbele kwa maslahi ya taifa lao hapana shaka taifa litaendelea. Inshallah Mungu Akipenda.

Hapana shaka kama nchi zote za Afrika zitachukua njia hii kwa hakika Afrika itapiga hatua kubwa ya maendeleo tena kwa kasi kubwa.

Nina uhakika kabisa kwamba, kama nchi za Kiafrika na watu wake wataungana na kutimiza yale yote yanayotakiwa na adili basi siku moja bara la Afrika litaibuka kuwa taifa lenye nguvu duniani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu hili liweze kutokea. Inshallah."(Salamu za pongezi za kuadhimisha miaka hamsini ya uhuru wa Tanzania bara alizotumiwa Raisi wa Tanzania Mheshimiwa Raisi Jakaya Mrisho Kikwete)



Raisi mstaafu wa awamu ya nne wa Tanzania
Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete

Niimani yangu wale wanaodhani kuondoka kwa mwalimu Nyerere kulikua ni anguko la kifira wataamsha tena hisia na harakati za ukombozi,watawala wetu waiangalia falsa upya ya ukweli na sababu za kupigania uhuru maneno ya Khalifa wa Jumuia ya Ahmadiyya duniani ni dawa tosha kwa kila mwenye kiu na madaraka hakika. Nionavyo mimi ili tumuenzi Mwalimu Nyerere kwa ufasaha kuna haja ya kukimbilia kisima hiki kisicha kauka yaani Ahmadiyya atakaye aje achote maji na aje mwisho tutaungana na Mola wetu mlezi.

Bustani ya Washairi

AHMADIYYA NA MAENDELEO YA KISWAHILI – TANZANIA

Na **Mahmood Hamsin Mubiru**

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Mama wa waaminio

171. Wakang'ara wafuasi,
Kwa kuyaacha maasi,
Wakawa kama fususi,
Thamani ilozidia.

172. Sala zao za vilio,
Hilo lao kimbilio,
Halikubaki salio,
La uchafu na udhia.

173. Mali zao wakatoa,
Kwa miradi ya Jalia,
Nazo zikasaidia,
Haki kuweza enea.

174. Wakatafuta elimu,
Wakenda kila sehemu,
Ni agizo la Hashimu,
Elimu kuzingatia.

175. Humo kwenye maulidi,
Kafanya kubwa juhudi,
Mambo yaliyo jadidi
Tumwa alituachia.

176. Daima tutakumbuka,
Mafunzo aliyoweka,
Ili tuweze kuvuka,
Tupate kuendelea.

177. Na yeye ndiye awali,
Mafunzo hayo jamili,
Ya haki pamwe adili,
Ili tupate tulia.

178. Mafunzo yenye thamani,
Ndiyo kwanza duniani,
Mafunzo hayo ya shani,
Binadamu kupokea.

179. La kwanza katuachia,
Umoja ameelezea,
Wa Mungu katuambia,
Ni Mmoja sio mia.

180. Muumbaji ni Ahadi,
Wala hanae walidi,
Ni yeye Mola Samadi,
Mwingine hatatokea.

181. Akaileta Kalima,
Ni tangazo la adhama,
Imara akasimama,
Shahada kushuhudia.

182. Kwa ghera ametangaza,
Tena kwa kufululiza,
Ni Mmoja katangaza,
Hilo la kuzingatia.

183. Kapinga ushirikina,
Ule wa baba na mwana,
Huo kasema hapana,
Ahadi Mola Jalia.

184. Katika ushirikina,
Upo wa kila aina,
Huo wote ameguna,
Hautufai insia.

185. Kuwaza unazonguvu,
Uwe ni mtu shupavu,
Ni mawazo yana kovu,
Shiriki umegusia.

186. Mola kumshirikisha,
Kosa kubwa la maisha,
Rabi ndiye Anatosha,
Yeye kumtegemea.

187. Kubwa letu kimbilio,
Katangaza azimio,
Nyote fanya kimbilio,
Kwenda kwa Mola Jalia.

188. Vilobaki upuuzi,
Kutusadi haviwezi,
Ila ni Mola Azizi,
Wa kuweza tuokoa.

189. Ibada ni kila kitu,
Sisi twaitwao watu,
Hapana hapana katu,
Hiyo kuiachilia.

190. Tusimamishe maombi,
Kwani maombi utambi,
Huunguza zetu dhambi,
Wasafi tukabakia.

191. Ukumbini ukifika,
Machozi yatiririka,
Kama ombi la baraka,
Rabi atakuridhia.

192. Ni dawa mujarabati,
Iletayo khairati,
Ukisujudu kwa dhati,
Uombalo hupokea.

193. Maombi ni muujiza,
Haja zako kutimiza,
Ibada kutekeleza,
Wajibu kwetu insia.

194. Funzo walisimamisha,
Na safina kuwavusha,
Safari kukamilisha,
Sharti lake ni dua,

195. Hino zawadi adhimu,
Alotupa muadhamu,
Tuitumie kwa hamu,
Ipate kutuokoa.

Usawa wa binadamu.

196. Usawa wa binadamu,
Katueleza Hashimu,
Sote wana wa Adamu,
Hakuna alozidia.

197. Rangi zetu si laana,
Mapenzi yake rabana,
Maua yakifanana,
Ni vigumu kuvutia.

198. Ila kwenye bustani,
Yanavutia machoni,
Na kuleta burudani,
Mengi yanapochanua.

199. Sote tuko sawasawa,
Kama sahani na kawa,
Kinyume chake si sawa,
Ubora kujidhania.

200. Na kigezo cha ubora,
Imani ilo Imara,
Ujitoapo kafara,
Rabi kumtumikia.

201. Ucha Mungu ni alama,
Ya kupendwa na Karima,
Ndiyo chanzo cha neema,
Siyo rangi nakataa.

202. Kayafuta majivuno,
Matajiri na wangano,
Kwetu kaacha mfano,
Haifai kubagua.

Haki za akina mama.

Utaendelea toleo Lijalo

ACHA OMBAOMBA

Isiwe sababu , yawee kuombaomba
Igiza ubabu, barabarani kuomba
Kisa wewe bubu, msaada kuuwomba
Acha ombaomba, Fanya unachokiweza

Kiwete sababu, juwani kujianika
Huwoni aibu, Wana Wakichakalika
Unajipa tabu, mikono kutotumika
Acha ombaomba, Fanya unachokiweza

Sifanye sababu, ulemavu lokushika
Lonacho jaribu, kuitafuta ruzuka
Mola takujibu, juhudi uloishika
Acha ombaomba, Fanya unachokiweza

Molawetu rabbu, hawapendi walochoka
Mali wasojaribu, kupokea wenyetaka
Wakosa thawabu, uwezo kutotumika
Acha ombaomba, Fanya unachokiweza

Masihi Omary Kisagwa
Dodoma

UA

Nafurahi kukuona, Machoni mwangu kipenzi,
Maradhi yangu hupona, Nikiwa nawe lazizi,
Na mwengine sijaona, Kuninyima usingizi,
Ua kipenzi cha Moyo, Mpenzi nikupendaye.

Ua umechanukia, Moyoni na kustawika,
Harufu ya kunukia, Kwako nimekamatika,
Ua na kufikiria, kila sa kila dakika,
Ua kipenzi cha Moyo, Mpenzi nikupendaye.

Ua langu Vumilivu, La himili hali zote,
Lenye hali ya tulivu, Daima kipindi chote,
Ua langu ni shupavu, Na zuri kwa Umbo lote,
Ua kipenzi cha Moyo, Mpenzi nikupendaye.

Ua mekuandikia, Na tamati mefikia,
Siishi kukusifia, Machoni wanivutia,
Sina pa kukimbilia, Kwako ndo nimezamia,
Ua kipenzi cha Moyo, Mpenzi nikupendaye.

Abubakary Abdallah Mwita. (Mkurya halisi.)

UMOJA NDIO SAFINA

Jina lako Rahman, ndio ninaloanzia
Naomba uniauni, niseme ninayofikiria
Wapulike wa pwani, Kigoma Dodoma pia
Umoja ndio safina, atokaye huangamia

Japo aone kichwani, akili zimetumia
Lakini huzama chini, maji yakamchukua
Huipoteza yakini, ataki akijililia
Umoja ndio safina, atokaye huangamia

Hivyo tuthamini, safina tulojipandia
Tusikae chocholoni , tuanze kuitoboa
Kuangamia yakini , lazima kutatokea
Umoja ndio safina, atokaye huangamia

Tuitoboe kwa nini , safina tuliojipandia
Vitu vilivyoduni , yafaa kuwaachia
Na mambo yenye thamani , yafaa kufikiria
Na vitatushusha chini , mkondo tatuchukua

Na wala usitamani , safinani kujitokea
N lazima ubaini , wewe utaangamia
Na uilewe auni , ushindwe jisaidia
Umoja ndio safina, atokaye huangamia

Hebu tulia safinani , usalama angalia
Na tena uwe makini , atakaeitoboa
Mulize kwa nini , nia ameng'ang'ania
Umoja ndio safina, atokaye huangamia

Tuingie maombini , kwa kujiombea
Tujaliwe kwa yakini, salama kuifikia
Na tufike kivukoni, Mola alokusudia
Umoja ndio safina, atokaye huangamia

Ewe Mola tuaini , waja wako tunalia
Sababu sisi ni duni, kusahau hutujia
Hivyo tulinde yakini, safina kutotoboa
Umoja ndio safina, atokaye huangamia

SHEKHE UMEPATA MWENZI

Mwamu Tahiri Marunda, nipe wako usikizi
Leo chati umepanda, umepata laazizi
Nami kungwi nakufunda, nikujuze viumbizi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Usichoke kumpenda, mwali ukambarizi.
Mpe ya ndani mawada, penzi limpe uchizi.
Awe Pete uwe chanda, muwe pacha wa mapenzi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Tulia na huyo dada, mithili ya mwenye ganzi
Mliwaze kwa kinanda, hata kwa gita la nyuzi.
Mhimize na ibada, ya Mola wetu Mwenyezi
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Useme naye kwa nyonda, simfanyie utwezi
Jihadhari kumdoda, kwa vifinyo na makwenzi
Na ili asije konda, jitahidi kumuenzi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Mpe upendo jadida, hakikisha humkwazi.
Sifia yake jasada, kwa mashairi na tenzi.
Umpambe kwa mashada, na libasi funikizi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Na makosa akitenda, usimpe shambulizi.
Mkanye kwa tafsida, na lugha ya ubembezi,
Jiepushe kumponda, maneno machukizi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Hata wakati wa shida, ipunguapo michuzi.
Kwa mapenzi hata binda, hunoga kama mkizi.
Mlishe ukimkanda, mwali asihisi ganzi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Ndugu zake kuwapenda, liwe jambo tangulizi.
Usiwafanyie inda, kwa upole uwaenzi.
Ndoa utaivurunda, usipokuwa mlezi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Mpe anchokipenda, simbanie tumizi,
Kwa bei kikikushinda, omba kwa Mola Azizi.
Subira na jitihada, na maombi ndo hirizi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Na kwenye ile kandanda, ya ndoa cheza kikazi.
Kimbiza kama kisinda, kimayele piga gozi,
Mechi hizo ukishinda, utaanzisha kizazi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Ninakuvika warida, ili ung'ae kimwezi.
Leo hutoranda randa, utazitunza pumzi.
Jioni ukale denda, na mke wako kipenzi.
Shekhe umepata mwenzi, usichoke kumpenda.

Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi).

KUNGURU

Ogopa aloshukuru, kwa yote uliyotenda
Wingi kakarakukuru, kumuachia kidonda
Usimanye uko huru, hutoonja chungu tunda
Majuto huja mwishoni, usicheze na kunguru.

Mahmood Hamsin Mubiru – Wamamba
Kiwalani - Dar es salaam.

FUMBO FUMBUENI

Nasema pole mpendwa, Mola akupe shifaa
Hofu maumivu kutendwa,Vyazua kizaa zaa
Tuyaonayo mageni, Fumbo siriye ni nini

Dua kwa wano tutoka, Waacha pengo huzuni
Twaacha kwenye vichaka, Wachanga Mola twauni
Tuyaonayo mageni, Fumbo siriye ni nini

Wanatungo wenye tenzi, Medani tokolezeni
Kwa utashi na mapenzi, Fumbo hili fumbueni
Tuonayo ni mageni, Fumbo siriye Ni nini

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga

Mti wa Tufaha



Hapo kale, kulikuwa na mti mzuri wa tufaha.

Mvulana mdogo alipenda kuja na kucheza karibu nayo kila siku. Alipanda juu ya mti. Alikula matufaha.

Alisinzia katika kivuli chake. Aliupenda mti na mti ulipenda kucheza naye.

Muda ulienda. Mvulana sasa alikuwa kijana na hakuwa tena akicheza karibu na mti tena.



Siku moja, mvulana alirudi kwenye mti na aligundua kuwa ulionekana kuwa na huzuni.

"Njoo ucheze nami" mti ulionekana kumurai kijana huyo.

"Mimi si mtoto tena, sichezi kwenye miti tena," mvulana akajibu. "Nataka vikorokoro vya kisasa. Nahitaji pesa kuzinunua."



"Pole, sina pesa, lakini unaweza kuchuma tufaha zangu zote na kuziuza. Kisha utakuwa na pesa." Mvulana alifurahi sana.

Alinyakua tufaha zote kwenye mti na kuondoka kwa furaha.

Mvulana hakurudi baada ya kuchuma tufaha. Mti ulihuzunika sana kwa mara nyingine tena.

Siku moja, miaka mingi baadaye, mvulana ambaye sasa alikuwa amegeuka kuwa mtu mzima alirudi na mti ukafurahi!

"Njoo ucheze nami," mti ulionekana kusema.

"Sina muda wa kucheza.



Lazima nifanye kazi kwa ajili ya mke wangu na watoto. Tunahitaji nyumba kwa ajili ya makazi. Unaweza kunisaidia?" yule mtu akajibu.

"Samahani, lakini sina nyumba yoyote. Lakini unaweza kukata matawi yangu ili kujenga nyumba yako."

Kwa hiyo mtu huyo alikata matawi yote ya mti kwa furaha na kuondoka zake kwa furaha. Mti ulifurahi kumuona akiwa na furaha lakini mtu huyo hakurudi kwa miaka na miaka. Mti ulikuwa tena wa upweke na umekasirika.

Siku moja ya kiangazi yenye joto kali, mwanamume huyo alirudi na mti ukafurahi.

"Njoo ucheze nami," mti ulionekana kusema.

"Nakaribia hamsini zangu. Ninataka kusafiri kwa meli ili niweze kupumzika wakati wa likizo yangu. Unaweza kunipa mashua?" aliuliza mtu huyo.



"Tumia shina langu kujenga mashua yako. Unaweza kusafiri mbali na kuwa na furaha," mti ulionekana kujibu.

Kwa hiyo mwanamume huyo alikata shina la mti kwa shangwe ili kutengeneza mashua. Alikwenda meli na hakutokea kwa muda mrefu.

Hatimaye, mwanamume huyo alirudi baada ya miaka mingi.

"Samahani kijana wangu. Lakini sina chochote kwa ajili yako tena. Hakuna matufaha zaidi kwako," mti ulionekana kusema.

"Hakuna shida, sina meno tena ya kuuma," mtu huyo alijibu.

"Hakuna shina tena la wewe kupanda," mti ulionekana kujibu.

"Mimi ni mzee sana kwa hilo sasa pia," mtu huyo alisema.

"Siwezi kukupa chochote kijana wangu. Kitu pekee kilichosalia ni mizizi yangu inayokufa," mti ulisema huku machozi yakimtoka.

"Sihitaji mengi sasa, mahali pa kupumzika tu. Nimechoka baada ya miaka hii yote," mwanamume huyo alisema.

"Safi! Mizizi ya miti mkuukuu ni mahali pazuri pa kuegemea na kupumzika, Njoo, uketi pamoja nami upumzike," mti ulionekana kunong'ona kimoyomoyo.



Mwanamume huyo aliketi kwenye nyasi, akiegemeza mwili wake dhaifu kwenye kisiki cha mti. Mti ulionekana kufurahi sana hadi kutabasamu kwa machozi...

Hii ni hadithi kwa kila mtu. Mti ni kama wazazi wetu. Tulipokuwa wadogo, tulipenda kucheza na Mama na Baba yetu. Tunapokua, tunawaacha… hurudi kwao tu wakati tunahitaji kitu au tunapokuwa na shida.

Haijalishi nini, wazazi wetu daima watakuwepo na kutoa kila walichoweza. Ili tu uwe na furaha.

Unaweza kufikiri kwamba mvulana huyo ni mkatili kwa mti huo, lakini hivyo ndivyo karibu sisi sote tunavyowatendea wazazi wetu. Tunawachukulia kawaida. Hatuthamini mambo yote wanayotufanyia, MPAKA wakati tumechelewa.

Allah **Atusamehe mapungufu yetu na atuongoze, Ameen**.

Wapende Wazazi wako....

"Na Mola wako Ameagiza kuwa msimwabudu ye yote ila Yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi; kama mmoja wao au wote wawili wakifikia uzee pamoja nawe, katu usiwaambie neno lo lote lenye kuashiria kwamba umechukia wala usiwakemee, bali zungumza nao kwa maneno ya ukarimu."

"Na uwainikie bawa la unyenyekevu kwa huruma. Na useme: Mola wangu, Uwarehemu kama walivyonilea katika utoto." Qur'an 17:24-25

Rasulullah^{saw} amesema Jibriyl^{as} kuwa.

"Ole wake yule ambaye wazazi wake au mmoja wao anafikia uzee mbele yao, na (kwa kushindwa kuwatumikia) haruhusiwi kuingia Jannah". Kwa hili Mtume (s.a.w.) alisema, *"Amin"*.

Jinsi ya kupika kuku aliyechanganywa na viungo (Tandoori/Sekela)

Na **Mtandao**



MAHITAJI

1. Kuku mzima 1
2. Kitunguu swaum/tangawizi
3. Maziwa ya mgando 1 kikombe cha chai
4. Curry powder ½ kijiko cha chai
5. Garam masala ½ kijiko cha chai
6. Coriander powder ½ kijiko cha chai
7. Cumin powder ½ kijiko cha chai
8. Chilli powder ½ kijiko cha chai
9. Limao ½
10. Chumvi kiasi
11. Rangi ya chakula nyekundu
12. Mafuta ya kupikia (vegetable oil) vijiko 2 vya chakula

JINSI YA KUTAYARISHA NA KUPIKA

1. Katakata kuku katika vipande vya kawaida kisha umuoshe na umkaushe maji vyema.
2. Baada ya hapo muweke katika bakuli kubwa na uanze kutia limao na spice zote kasoro mafuta, mtindi na rangi ya chakula.
3. Changanya spice na kuku mpaka vikolee vizuri. Baada ya hapo changanya mtindi na rangi ya chakula pembeni na kisha umwagie katika kuku na uchanganye tena vizuri.
4. Baada ya hapo malizia kwa kutia mafuta na uchanganye vizuri kisha funika na uweke katika friji kwa muda wa masaa 3 ili kuku aingie viungo.
5. Baada ya hapo muoke kuku wako kwa muda wa nusu saa katika moto wa 200°C. Baada ya hapo kuku wako atakuwa tayari kwa kuliwa.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA*as*

Dini za Dunia

Miongoni mwa kanuni ambazo nimefanywa niziamini kwa dhati ipo moja ambayo imefunuliwa kwangu mahsusi na Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Kanuni yenyewe ni kutosema ni za asili ya ubandia zile aina za dini ambazo zilifunuliwa na Mungu kwa njia ya manabii Wake na ambazo zina alama hizi: Zimepata kukubaliwa sana katika maeneo fulani ya dunia; baada ya kushinda kila aina ya upinzani, zimepata mafanikio na ustawi mkubwa. Baada ya kudumu kwa muda mrefu, zimepata kuwa alama ya zama zao na sura ya mafanikio. Sawa na kanuni hii, dini kama hizo yamkini zilikuwa dini za kweli na bila shaka waanzilishi wao walikuwa mitume wa kweli wa Mwenyezi Mungu.

(Rhoohani Khazain Jal. 12, Uk. 256: Tohfae Quisariya Uk. 4)

KUTOKA MAKTABA

Na Ally Hamisi Mbambwa

Mzee Mwishehe Juma

Mwishoni mwa miaka ya Khamsini, bila shaka ni miaka ya kukumbukwa mno na Wakazi wa Tarafa ya Mkuyuni – Morogoro vijijini kutokana na changamoto ya kielimu iliyoibuliwa na Kijana mdogo dhidi ya masheikh wabobevu wa tarafa hiyo.

1. Sheikh Chang'walo – Sheikh wa Tarafa ya Mkuyuni
2. Sheikh Ramadhani Khalfan – Sheikh wa kata ya Luholole
3. Sheikh Rajabu Chande – Sheikh wa kijiji cha Ving'ongo na
4. Sheikh Sewando – aliyekuwa sheikh wa kijiji cha Mfumbwe.

Masheikh hawa walikesha tongomacho wakitafakari njia gani mujarrabu waitumie kumnyamazisha na kumshikisha adabu kijana ili aache kuwakufurisha.

Ndipo walipoamua kuungana pamoja na kuitisha mjadala wa wazi katika tarafa hiyo dhidi yake.

Akipinga bidaa za Hitima, talakini, matanga na upotofu mwingine ulionasibishwa na Dini tukufu ya Islam.

Kijana alikuwa amerudi kutoka masomoni Zanzibar kujifunza elimu ya dini ya Kiislam kwa miaka mitano toka mwaka1950 hadi 1955.

Alipata elimu yake Katika Madrasa ya Bi Fatuma Bakari ambapo alijifunza elimu ya Fiq'hi, Kujua na kuelewa kwa undani nguzo za Imani na nguzo za Islam pia alifundishwa hoja za kupinga upotofu wa bidaa zilizoingizwa katika dini Tukufu ya Islam sawa na hadithi za Mtume Muhammad s.a.w.

Elimu aliyoipata, ailiifanyia kazi kwa vitendo kwa kuiasa jamii yake ya Mkuyuni . Aliwaambia waachane na itikadi potofu zilizo kinyume na mafundisho sahihi ya Islam kama vile, hitima, matanga, maulidi za kuchanganyika wanawake na wanaume n.k.

Badala ya furaha kwa kumpokea mwana wao aliyekwenda kutafuta elimu katika kitovu cha elimu wakati huo, ndugu na jamaa hususani wazazi walifadhaishwa na kukasirishwa sana na mwenendo wa kijana wao. walimuasa aache kuwakufurisha, lakini hakuwasikiliza. Hatimaye baba yake akamfukuza nyumbani na jamii ikajitenga kushirikiana naye.

Aliyapokea kwa mikono miwili maamuzi hayo ya wazazi na jamii yake kwa sababu aliamini amesimama katika upande wa haki.

Akaamua kwenda kuishi msituni katika vilele vya milima ya uluguru. Na kutoka huko milimani, aliongeza mashambulizi ya kupinga itikadi potofu zilizoingizwa ndani ya dini tukufu ya Islam, ndipo masheikh wale wakaungana kuitisha mjadala dhidi yake ili wamshikishe adabu.

Maelezo haya, hayawezi kunasibishwa kwa mtu mwingine yeyote bali kwa mtu aliyekuwa *mtii sana, mpole sana, mcheshi na mwenye tabasamu muda wote, mwenye upendo, mwenye bidii ya kazi na muhubiri mkubwa*, huyu si mwingine bali *Mzee Mwishehe Juma Waziri Kiosi* aliyezaliwa mwaka 1934 katika kijiji cha Lung'ala, kata ya Kinole tarafa ya Mkuyuni Morogoro vijijini.

Bi. Mwajabu Binti Mwishehe, alijiona kwenye njozi kwamba; "yupo katika chumba fulani akiwa kwenye harakati za kujifungua. Kisha akaona kwamba amejifungua mtoto wa kiume, kisha akasikia sauti ya baba yake kutoka nje akiuliza; mbona nasikia sauti humo ndani? Mama huyo akamjibu kwamba kuna mdogo wako – yaani mjukuu wako humu ndani. Babaake akamjibu kwamba ikiwa kuna mjukuu wangu humo ndani basi apewe jina la 'Mwishehe' na alisisitiza hivyo mara tatu".

Bi Mwajabu alipoamka usingizini alimsimulia mumewe mzee Juma Waziri Kiosi. Ndipo baada ya miezi michache kupita, yaani mwanzoni mwa mwaka 1934 mama huyo alijifungua mtoto wa kiume na akapewa jina lilelile la Mwishehe kulingana na ndoto ile.

Kujiunga na Jumuiya

Itaendelea Inshallah

MATUKIO KATIKA PICHA





Mahafali ya Shule ya msingi Ahmadiyya iliyopo Kihonda, Morogoro ambayo Amir na Mbashiri Mkuu aliyabariki kwa uwepo wake.



Naibu Amir Sh. Abdulrahman Ame akikabidhi kombe kwa kapteni wa timu iliyoibuka bingwa Msongola Veterans aliposhiriki fainali na ufungaji wa kombe hilo maarufu kama Ahmadiyya Cup



Mhe. Omary Juma Kipanga, Naibu Wazir Elimu, Sayansi na Teknolojia akihutubia washiriki wa Jalsa Salana Tanzania 2022 alipokuwa mgeni rasmi wa kikao cha pili cha Mkutano huo



Muonekano wa banda la vitabu katika maonyesho ya Jalsa Salana Tanzani 2022



Mkutano na waandishi wa habari kwa ajili ya kuitangaza Jalsa Salana Tanzania 2022





Waziri wa Nchi Sera, Bunge na uratibu Mh. George Simabchawene alishiriki kikao cha kwanza cha Mkutano wa Mwaka wa 51 - Jalsa Salana Tanzania 2022. Kulia akihutubia wahudhuriaji na kushoto akipokea zawadi ya vitabu toka kwa Amir na Mbashiri Mkuu Sh. Tahir Mahmood Chaudhy

Amir sahib agawa vyeti kwa wahitimu darasa la saba

Na **Mwl Shamhuni Juma**
Jamia Ahmadiyya, Morogoro

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu Jumuiya ya Waislamu waahmadiyya Siku ya al-hamisi tarehe 22 September Mwaka 2022, imepiga hatua nyingine mbele katika nyanja ya Kielimu. Siku hiyo historia imewekwa nchini. pale ambapo Amiri na Mbashiri mkuu - Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib alipowatunuku vyeti wahitimu wa elimu ya msingi Katika mahafali ya shule ya Ahmadiyya ya pili ya Shule yetu iliyoanza Mwaka 2013 Katika eneo la Jamia, na hadi Sasa Shule ina vyumba takriban Kumi (10) Vya madarasa, vyumba vitatu vya utawala na vingine vya madarasa pamoja na ukumbi mmoja mkubwa; Aliongezea kwa kusema kuwa asilimia Thelathini na tatu (33%) ya wanafunzi wanapata punguzo la ada, na zaidi ya hayo ada inayotozwa Katika shule yetu ni nafuu zaidi kuliko shule ningi za pembezoni. Baada ya maelezo hayo, ilifuata risala ya Wanafunzi



Amir na Mbashiri mkuu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib akitunuku cheti cha kuhitimu elimu ya msingi kwa mwanafunzi wa Shule ya msingi Ahmadiyya iliyopo Kihonda, Morogoro

iliyopo Kihonda Katika Manispaa ya Morogoro.

Hafla ilianza majira ya saa 3 asubuhi, ambapo Amir Sahib aliwasili shuleni akifuatana na viongozi mbali mbali wa jamaati akiwemo Sh Abid Mahmood Bhatti Sahib Naibu Amiri na Mkurugenzi wa Shule ya Ahmadiyya Morogoro, Sh Abdur rahman Ame Sahib Naibu Amiri, Sh Karim u deen Shams Sahib Sheikh wa mkoa morogoro, na pia Sh Abdul Nasir Momin Sahib msaidizi wa mkurugenzi wa shule. Viongozi hao walipokelewa kwa gwaride maalum lililongozwa na Skauti wa Shule chini ya mwalimu Ramadhani Mziray.

baada ya kukagua gwaride, Amir sahib na wajumbe wake wakaelekea ukumbini. Hafla ikaanza na usomaji wa Qurami tukufu ambayo ilisomwa na mmoja wa wanafunzi wahitimu aitwaye Yusuf Ally Makame na kisha kufuatiwa na wimbo wa Taifa na wimbo maalum wa shule.

Kisha yalifuata maelezo machache juu ya maendeleo ya shule ambayo yalitolewa na Mwl Omari Bashir Mwalimu wa taaluma.

Katika maelezo yake mwalimu alisema kuwa hii ni mahafali (Wahitimu) ambayo ilisoma na Mwanafunzi aitwaye Zaujia Salimu Muhando

Katika risala yao wahitimu walisema kuwa Wanaushukuru uongozi wa shule na taasisi nzima ya Jumuiya ya Ahmadiyya Kwa huduma nzuri walizopata kielimu pamoja na malezi mema, Kwa muda wote waliokuwa hapa shuleni.

Baada ya risala hiyo ya wahitimu lilifuata zoezi la kugawa vyeti kwa wahitimu. Mheshimiwa Amir na Mbashiri mkuu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib aligawa vyeti hivi, na kutoa nasaha chache kwa wanafunzi. Katika maongezi yake mgeni rasmi alitoa nasaha zenye kujenga maadili mema na Khulka bora, pia Amir Sahib aliwataka wahitimu kudumisha nidhamu na khulka bora na kuepuka makundi na mienendo isiyofia ambayo hupelekea mmomoonyoko wa maadili katika Jamii.

Aliwataka wawe waungwana na raia wema kwa familia na Taifa kwa ujumla. Amir Sahib aliongoza maombi ya Kimya na Kufunga hafla hiyo. Mwisho washiriki wote wa hafla hiyo walihudumiwa vinywaji.

Tafsiri ya Ujumbe wa Hadhrat Khalifatul Masih kwa Ajili ya Jalsa Salana ya 51 Tanzania

Ndugu Wanajumuiya wa Ahmadiyya Muslim Jama'at Tanzania

Assalaam alaikum warahmatullah wabarakaatuh.

Nimefurahishwa sana kuwa mnafanya Jalsa Salana yenu ya Mwaka wa 51 kuanzia tarehe 30 Septemba hadi tarehe 1 na 2 Oktoba 2022. Mwenyezi Mungu aibariki Jalsa yenu kwa mafanikio makubwa na wale wote wanaoshiriki wapate baraka kubwa za kiroho, waongezeke katika ujuzi na ufahamu wa dini yetu ya Islamu na waweze kuongezeka na kusonga mbele katika imani, matendo mema na Uchamungu.

Mnapaswa kuleta mabadiliko ya Uchamungu ndani yenu. Hamtakiwi kuridhika tu na ukweli kwamba mumemkubali Masihi Aliyeahidiwa ambaye kuja kwake hakukutabiriwa na yeyote isipokuwa na Mtukufu Mtume wetu Muhammad (saw) mwenyewe, bali lazima mujitahidi kwa uwezo wenu wote kufuata masharti ya Bai'at yenu, na kwa kutumia uwezo wenu wote na vipaji vyenu, mjirekebishe kwa kudumu na kuinua hali zenu za kiroho. Kuhusiana na hili, Masihi Aliyeahidiwa (as) amesema:

'Madhumuni hasa ambayo Mwenyezi Mungu ameianzisha Jumuiya hii ni kwa ajili ya ufahamu wa kweli wa Mungu ambao umetoweka katika ulimwengu huu na kwa ajili ya Uchamungu wa kweli na usafi ambao haupatikani tena katika siku hizi na enzi hizi, uanzishwe kwa mara nyingine.' {Malfuzat, Vol. 7, ukurasa wa 277-278}

Kwa hivyo, ikiwa tunataka kujirekebisha, basi ni lazima tuweke nukta hii mbele ya akili zetu, kwamba tutajaribu kutekeleza kila tendo jema na la utawa, na kwamba tutafanya kila tuwezalo kuepuka kila tendo ovu na la dhambi. Ikiwa Bai'at yetu ni ya kweli, na lengo letu ni kubadilisha ulimwengu, basi ni lazima tuwe macho kiroho kuhusiana na kuendeleza fadhila za Uchamungu ndani yetu. Kwa hivyo, zingatieni Sala zenu tano za kila siku na swalini Swala zenu kwa kudumu na kwa jamaa na jaribuni kuanzisha mahusiano ya karibu na ya dhati na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ninawakumbusheni juu ya jambo muhimu na la msingi kuhusu taasisi ya Kimbingu ya Khilafat-e-Ahmadiyya ambayo inatupa baraka zisizohesabika. Tunapaswa kujaribu kujenga mafungamano thabiti na Khalifatul Masihi na kubaki waaminifu kabisa katika hali zote. Tunapaswa pia kuwafundisha watoto wetu juu ya umuhimu wa Ukhalifa na tuhakikishe kwamba vizazi vyetu vijavyo daima vinabaki ndani ya mwongozo uliobarikiwa, chini ya mwavuli na ulezi wa Ukhalifa.

Kumbukeni kwamba, mustakabali wa Uislamu na ukuzwaji wa amani duniani vyote vinategemea Khilafat-e-Ahmadiyya. Katika suala hili, namshauri kila Ahmadiyya kutazama MTA mara kwa mara na kufaidika nayo. Hasa, mnapaswa kusikiliza mara kwa mara hotuba za Ijumaa na hotuba zangu za matukio mengine. Hakika, MTA ni chombo bora kabisa kinachokuunganisheni moja kwa moja na Ukhalifa.

Ulimwengu uko katika hatua mbaya. Kwa hakika, suluhisho pekee la mgogoro uliopo ni kwa wanadamu kumtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumwelekea Muumba wao na kuwa chini ya ulinzi na hifadhi ya Imam wa Zama, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi (as). Kwa hiyo, ni muhimu kwamba muongeze juhudi zenu za kuhubiri na kueneza ujumbe wa kweli na wa amani wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya sehemu mbali mbali. Katika suala hili, mnapaswa kupanua kwa kiasi kikubwa na kuendeleza mipango yenu ya Tabligh ili muweze kuwaalika watafutaji wengi zaidi wa ukweli kufahamu na kukubali mafundisho mazuri ya Uislamu Ahmadiyyat.

Mkiwa washiriki mliobahatika wa Jalsa, nyinyi ndio wapokeaji maalum wa maombi ya dhati na ya ikhlas ya Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye amewaombea mahsusi wale wanaosafiri kwenda kuhudhuria Jalsa kama ifuatavyo:

Namalizia kwa maombi ya kwamba kila mwenye kusafiri kwa ajili ya (kuhudhuria) Mkutano huu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu: *Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, awe pamoja naye, amlipe malipo makubwa, amrehemu, amfanyie wepesi hali yake ya shida na wasiwasi na kuondoa uchungu na huzuni yake. Ampe njia ya kutoka katika kila dhiki na amfungulie njia za [kufikia] malengo yake anayoyapenda, na amhuishe, Siku ya Kiyama, miongoni mwa waja Wake ambao ni wenye kupokea baraka na Rehema Zake. Na awe Mlinzi wao kutoka kutokuwepo kwao mpaka baada ya kumalizika safari yao. Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Mtukufu na Mpaji wa fadhila, Mwingi wa kurehemu na Mwenye Kusuluhisha matatizo yote, Tukubalie maombi haya yote, na Utujaalie Ushindi juu ya wapinzani wetu kwa ishara zinazong'aa, kwa sababu Wewe peke yako Ndiwe Mwenye uwezo na nguvu zote. Ameen! Ameen!!'*

{lshtihar 7 Des. 1892, Majmuu'ah lshtiharat Juz. Mimi, Ukurasa 342]

Mwenyezi Mungu aibariki Jalsa Salana yenu kwa mafanikio makubwa na akuwezesheni kuleta mageuzi ya kweli katika maisha yenu kuelekea uchamungu zaidi, tabia njema, matendo mema na huduma ya Uislamu Ahmadiyyat na ubinadamu. Mwenyezi Mungu awabarikini nyote.

Wassalam

Wenu mwaminifu,

MIRZA MASROOR AHMAD

KHALIFATUL MASIH V

Ushindi mkubwa kwa wanadamu wote

Masimulizi ya Baraka za Ziara ya Khalifa Mtukufu Marekani 2022

Kutoka uk. 12

Mwenyezi Mungu Aendelee kuzidisha ikhlasi na kujitolea katika nyoyo za Waahmadiyya wote.

Hisia na Athari ya Wageni

Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba atawasilisha hisia za wageni mbalimbali wasiokuwa Waahmadiyya kutoka katika ziara hii.

Khalifa mtukufu*atba* alimnukuu Meya wa Zion ambaye alisema kwamba ilikuwa ni heshima kwake kumkaribisha Khalifa mtukufu*atba* huko Zion. Amesema kauli mbiu ya Zion ni '***historic past and dynamic future***' (Mapitio ya kukumbukwa na mustakabali wenye kheri) na msikiti wa Zion ni mfano kamili wa hilo. Alisema kwa uzinduzi wa msikiti huu mpya, ana matumaini makubwa na mustakabali wa mji huu unaohusishwa na msikiti huu na Jumuiya ya Ahmadiyya. Kisha Meya alikabidhi pia alama ya ufunguo wa jiji hilo kwa Khalifa mtukufu*atba*. Pia alieleza kwamba Khalifa mtukufu*atba* ulimwacha akiwa hana la kusema.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kuwa Mjumbe wa Bunge la Illinois Mhe. Joyce Mason alisema Alexander Dowie alitaka kuanzisha jamii ya kitheokrasi (ubaguzi wa kidini), hata hivyo



Alexander Dowie

leo, Zion ni makazi ya watu kutoka asili tofauti na msikiti huu mpya ni alama kubwa ya hilo. Aliipongeza Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kwa ushindi huu mkubwa.

Khalifa mtukufu*atba* alimnukuu Katrina Lantos ambaye alisema ilistaajabisha kusikia jinsi tambio la maombi lilivyovutia licha ya kwamba vyombo vya habari vya kielektroniki havikuwepo wakati huo. Alisema kuwa kuanzishwa kwa msikiti huu kunaonyesha wazi ni nani alishinda katika tambio hilo la maombi; hata hivyo huu haukuwa ushindi kwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya tu bali kwa wanadamu wote.

Khalifa mtukufu*atba* alimnukuu Dk. Craig Considine – profesa Mkristo ambaye ameandika kumhusu Mtukufu Mtume (saw) – ambaye alisema kwamba aliheshimiwa kukutana na Khalifa mtukufu*atba* na kwamba alijifunza mengi kuhusu Uislamu kutoka hotuba ya Khalifa mtukufu*atba*. Alisema kwamba namna Khalifa mtukufu*atba* alivyozungumza juu ya mada ya Uislamu ilikuwa rahisi kueleweka kwa kila mtu. Pia alikuwepo kusikiliza khutba yake ya Ijumaa na akasema kwamba hajawahi kusikia khutba kama hii hapo kabla.

Khalifa mtukufu*atba* aliwasilisha hisia za wageni wengine mbalimbali kutoka Zion, wakiwemo viongozi wa kuchaguliwa, walimu, wafanyakazi wa huduma za dharura na wengineo ambao walionyesha heshima yao kwa Khalifa mtukufu*atba* na ujumbe aliowasilisha, umoja na maelewano ambayo alihimiza na namna alivyowasilisha historia ya Zion na mafundisho ya Uislamu.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kuwa msikiti wa Baitul Ikram ulizinduliwa huko Dallas na uzinduzi huo ulihudhuriwa na wageni 140. Mjumbe wa Baraza la Jiji la Allen, Carl Clemencich alikabidhi ufunguo wa jiji kwa Khalifa mtukufu*atba* na akaelezea shukrani zake kwa kazi ya kibinadamu iliyofanywa na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Alisema kuwa mji wa Allen ulikuwa na bahati kubwa kwamba Jumuiya hiyo ya amani na ubinadamu imejikita katika mji huu.

Khalifa mtukufu*atba* alimnukuu Prof Dr Robert Hunt, Mkurugenzi wa Idara ya Theolojia ya Ulimwengu katika Chuo Kikuu cha Southern Methodist cha Perkins School of Theology, ambaye aliishukuru Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kwa kumwalika yeye na wenzake. Alimpongeza Khalifa mtukufu*atba* kwa kukuza uhuru wa kidini na mazungumzo baina ya dini.

Khalifa mtukufu*atba* alimnukuu Mbunge wa Republican Mhe. Michael McCaul ambaye alisema kwamba Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inaonyesha jinsi imani za Ibrahimu zinavyoweza kuishi pamoja kwa upatano. Alisema yuko mbioni kusoma kitabu cha *Jesus in India* na atafanya utafiti zaidi. Alisema mengi tunaweza kujifunza kutoka kwa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kuhusu amani, wema na upendo. Alipongeza juhudi za Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kueneza amani, kuanzisha umoja, na kukomesha itikadi kali na kupambana na umaskini.

Khalifa mtukufu*atba* alimnukuu mgeni kutoka Kanisa la Presbytarian la Kaskazini ambaye alisema kwamba hajawahi kuona mtu yeyote akijitahidi kama Khalifa mtukufu*atba* kwa ajili ya kuanzishwa kwa amani duniani. Alisema kama watu wangesikiliza hotuba hii badala ya kupora haki za majirani zao na wenzao basi amani ingeweza kuimarika.

Khalifa mtukufu*atba* aliwasilisha maoni na hisia za wageni wengine mbalimbali kutoka Dallas ambao walionyesha shukrani zao kwa juhudi za Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kupenda amani na athari ya kutia moyo ya hotuba ya Khalifa mtukufu*atba* ambayo ilionyesha jinsi amani ya kweli, umoja na kuheshimiana pamoja na upendo unavyoweza kuimarishwa.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kuwa jengo kubwa pia lilizinduliwa huko Fort Worth, Texas ambapo inapangwa kujenga kuba na minara miwili ili kuligeuza kuwa msikiti. Khalifa mtukufu*atba* alisema kuwa ni jengo zuri ambapo siku moja aliongoza swala ya jioni.

Khalifa mtukufu*atba* alinukuu hisia za mgeni kutoka Fort Worth ambaye alisema kwamba Khalifa mtukufu*atba* aliwasilisha ujumbe bora kabisa na hasa akampongeza Khalifa mtukufu*atba* kwa onyo alilotoa kwamba yeyote ambaye atashiriki katika vita vya dunia bila shaka ataangamizwa.

Kufikiwa na Kufanyika kwa Shughuli Mbalimbali nchini Marekani

Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba kulikuwa na maonyesho huko Zion yanayohusu Tambio la Maombi. Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) alitaja kwamba alijua magazeti 32 ambayo yalitaja tambio hilo la maombi, lakini akasema kwamba alikuwa na hakika kwamba kuna mengi zaidi. Baada ya utafiti zaidi, Jumuiya ya Marekani ilipata sehemu 128 zaidi za habari kutoka wakati wa Masihi Aliyeahidiwa (as) na kufikisha jumla ya 160.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kuwa vyombo vya habari vya Marekani pia viliripoti uzinduzi wa msikiti wa Zion, ikiwa ni pamoja na Associated Press ambao waliandika makala yenye kichwa ***Mitume Wawili na Tambio la Maombi la Karne moja iliyopita lasisimua msikiti wa Zion***. Kulingana na tovuti yao wasomaji wake ni karibu nusu ya idadi ya watu duniani. Makala haya yalichapishwa katika vyanzo 412 katika nchi 13, ikiwa ni pamoja na *Washington Post, ABC News, Toronto Star, The Hill* na magazeti mengine mengi maarufu.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kuwa magazeti 9 mashuhuri, machapisho 6 ya mtandaoni na vituo vya redio nchini Canada pia viliripoti uzinduzi wa msikiti huko Zion. Uzinduzi huu pia ulitangazwa nchini Uingereza, Sierra Leone, Taiwan, India, Hong Kong, Peru, Ufilipino, Afrika Kusini, Tanzania na Vietnam.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kuwa MTA Afrika pia ilitoa matangazo Mubashara ya hotuba za Khalifa mtukufu*atba* kutoka Zion na Dallas. Ripoti mbalimbali za habari pia zilitayarishwa kwa ajili ya idhaa za ndani katika sehemu mbalimbali za Afrika. Mwanajamaat mpya wa Ahmadiyya kutoka Sierra Leone alisema kwamba kama angetambua kuhusu tambio hili la maombi na Alexander Dowie na ushindi uliofuata wa Masihi Aliyeahidiwa (as), basi angekuwa amejiunga miaka 20 iliyopita.

Khalifa mtukufu*atba* pia alitaja mikutano yake na Waahmadiyya wapya na akazungumzia baadhi ya mapambano na upinzani ambao wamekabiliana nao. Kutokana na maombi ya wanajumuiya wapya, kulikuwa na tukio la Uchukuaji wa Bait ambalo lilifanyika.

Khalifa mtukufu*atba* alisema kwamba kwa rehema za Mwenyezi Mungu, safari hii ilimiminiwa baraka Zake na akaomba Baraka za Mwenyezi Mungu ziendelee kutunyeshea.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAB.I-RAB.II 1444 AH | NOVEMBA 2022 | NUBUWWAT 1401 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Mtukufu Mtume Muhammad^{saw} alisema: ***Mbora wenu ni ambaye ni mwema zaidi kwa kulipa deni.*** **(Kashful-Ghummah).**

Ushindi mkubwa kwa wanadamu wote

Masimulizi ya Baraka za Ziara ya Khalifa Mtukufu Marekani 2022

Katika hotuba ya Ijumaa ya Tarehe 21 Oktoba, 2022; Baada ya kusoma Tashahhud, Tawwudh na Surah Al Fatiha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih wa Tano^{atba} alisema hivi karibuni, alitembelea Marekani na kwa rehema za Mwenyezi Mungu safari hii ilikwenda vizuri.

Khalifa mtukufu^{atba} alisema wanajumuiya walipokea habari kupitia MTA na vyombo vingine vya habari vya kielektroniki, vikiwemo vyombo vingine mbalimbali vya habari pia. Baraka za Mungu Mwenye Enzi zilionekana kila pembe katika ziara hii, zikileta athari chanya sio tu kwa Waahmadiyya, bali na kwa wengine pia. Kulikuwa na kijana mmoja ambaye alimwambia rafiki yake kwamba alikuwa na mashaka fulani kuhusu Ahmadiyya na Khilafat ambayo yaliondolewa kabisa kutokana na ziara hii. Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba kulikuwa na mifano mingi kama hii.

Upendo na Unyofu wa Waislamu wa Waahmadiyya nchini Marekani

Khalifa mtukufu^{atba} alisema



Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} akihutubia Ijumaa katika msikiti wa Bait-ur-Rahman, Maryland, Marekani alipokuwa ziarani

kwamba huko Zion, Dallas na Baitur Rahman, Maryland kuliendelea kuwa na idadi kubwa ya wanaume, wanawake na watoto waliokusanyika kwa ajili ya Sala. Hisia na mawazo waliyoeleza wakati Khalifa mtukufu^{atba} akitembea kwenda na kurudi msikitini zilionyesha wazi kwamba wana mapenzi ya kweli kwa Ukhalifa ndani ya mioyo yao. Watu walikuwa wakipanga foleni kwa saa nyingi ili tu kuingia msikitini kwa ajili ya Sala. Hii inaashiria wazi kwamba kwa neema ya Mwenyezi Mungu watu hawa wana mapenzi kwa imani yao na Ukhalifa. Watoto wangesimama kwenye foleni kwa saa tano hadi sita kwani pia kulikuwa na ukaguzi mbalimbali, lakini hakuna aliyelalamika. Mgeni fulani huko Zion hata alitoa maoni jinsi kila kitu kilivyokuwa kikiendelea vizuri na licha ya ukaguzi mbalimbali uliowekwa, hakuna aliyelalamika.

Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba wazazi wa mtoto wa miaka 11 au 12 walimwambia kwamba mtoto wao alikuwa anapanga foleni saa kadhaa kabla ya swala, ilhali hakuwahi kuzingatia kwa ukaribu sana sala zake hapo awali. Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba aliona mapenzi makubwa na ikhlasi kwa watoto pia. Khalifa mtukufu^{atba} aliomba kwamba shauku hii ya Sala ambayo ilikuwa dhahiri ibakie daima na misikiti hii ibaki kuwa na watu wengi.

Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba katika mahala pa kidunia kama Amerika, watu wanaweza kufikiri kwamba hakuna umakini unaotolewa kwenye imani, hata hivyo Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba aliona kinyume chake kwa Waahmadiyya aliowaona katika safari hii. Katika kila kituo kulikuwa na watu wengi zaidi kuliko ilivyotarajiwa. Kwa kweli, huko Baitur Rahman Maryland, wakati mwingine idadi ilizidi hata ile ya mkutano wa mwaka (Jalsa Salana). Khalifa mtukufu^{atba} aliomba kwamba

Endelea uk 11

KITABU KIPYA



Majibu ya Maswali Manne ya Mkristo Sirajuddin

Hii ni tafsiri ya Kiswahili ya Siraj-ud-Din 'Isaa'ee Ke Chaar Sawaalon Kaa Jawaab kilichoandikwa na Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad, amani iwe juu yake. Kitabu hicho kinakazia imani zifuatazo katika kujibu maswali ya Mkristo:

- Mafundisho ya Kikristo ya Toba kwa njia ya kile kinachoitwa dhabihu iliyolaaniwa ni chukizo na kufuru dhidi ya Nabii mpendwa wa Mungu.
- Yesu, amani iwe juu yake, hakufa msalabani na hakuwahi kulaaniwa.
- Quran Tukufu imekamilisha dhana ya Tauheed (Upweke wa Mungu), ingawa pia ilikuwa ni kanuni ya msingi katika maandiko yaliyotangulia.
- Mafundisho ya kiulimwengu ya Kurani Tukufu ni kwa watu wote na nyakati zote, ambapo maandiko ya awali yaliweka mafundisho yao kwa watu maalum kwa nyakati maalum.
- Uislamu unaamrisha kumpenda Mungu pekee, na kuhusiana na wanadamu unafunza rehema na huruma.
- Vita vilivyopiganwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw), rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, vilikuwa vya kujihami kimaumbile na havikukusudiwa kulazimisha Uislamu kwa wengine.

Haya ni baadhi ya mafundisho ya hali ya juu ambayo yaliianzisha Ahmadiyya katika vuguvugu la wamishionari wa Kiislamu duniani kote ambavyo iko leo.

Jipatie nakala yako kwa bei ya Tsh 2,500/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com